# *Joho La Kuachiwa*

Nilikuwa ndani pamoja na mchungaji hivi punde. Nikasema . . . Nilimwomba jana anipigie simu. Nikaja kugundua, nilininii tu . . . Siku nzima, hakukuwako na simu, nami nikawazia, "Vema, sijui kuna nini? Kitu fulani ni . . . Kila kitu ni shwari kabisa." Na baada ya kitambo kidogo, Dada Wood akaja na simu chache. Simu yangu ilikuwa imezimika, kwa hiyo, kama yeyote kati yenu alikuwa amepiga simu. Simu ililia, lakini haingetoa mwangwi mle ndani, kwa hivyo shida ilikuwa chini kwenye mtambo wa kuunganishia. Waliirekebisha yapata saa mbili jana usiku, ama labda mapema kidogo, na, simu, simu zinaingia sasa.

2 Tuna furaha kuwa katika ibada asubuhi ya leo. Nilishikwa na mafua makali, ambayo kwa kawaida hunishika ninaporudi nyumbani. Ninatembea kwa shida katika theluji iliyofikia kiunoni, na kulala nje usiku. Siiwazii ninapokuwa mbali na hapa, bali mara nikivuka tu kile kilima kule New Albany, ndiyo tu unayopaswa kufanya, kuingia katika bonde hili, ndipo ninashikwa na mafua makali. Na ni ninii . . . Sijui, kuna kitu fulani mumu humu bondeni hapa ambacho kinaiweka chini. Na iko chini, wala haikubaliani nami hata kidogo.

3 Sasa, tuna furaha kuwa kanisani, kama nilivyosema, na kuwa tukimsikia mpendwa mchungaji wetu mwema akituombea dua, na kwa Bwana Yesu. Na—na kusikia, inasikitisha kusikia wagonjwa na wahitaji wengi sana, na jinsi Shetani anavyofanya mashambulizi ya kumfanya kila mtu awe mgonjwa.

4 Na maskini mama mmoja alisimama kuhusu dada yake kule nyuma, nami ninamjua Dada Sauer huko chini alikuwa pamoja naye. Daktari alimwacha aende nyumbani akafe sasa. Naye angali anaamini atapona. Na ni mahututi sana, sana. Mama mkwe wangu, vivyo hivyo, umri wa miaka sabini sasa. Ni mahututi sana. Na bila shaka magonjwa mengi kote nchini. Na halafu kuna Roho Mtakatifu kote nchini, mnaona, anayeponya magonjwa yetu, endapo tu tunaweza kupata fadhili Kwake.

5 Na sasa, kwa kuwa koo langu linauma, haliumi, lakini lina vidonda. Nami sitajaribu kuhubiri, bali kuongea nanyi kwa muda kidogo tu kutoka kwenye Neno, na kisha tuingie kuwaombea wagonjwa, ambalo niliahidi kufanya. Lakini kabla tu ya kufanya hivi, ningependa kutangaza mikutano mingine zaidi. Mimi . . .

6 Katika ibada zangu nimekuwa na upinzani kidogo wa . . . si upinzani, bali ni kutokueleweka kidogo tu. Na mara nyingi, mimi—mimi sina njia za kueneza huduma yangu, kama—kama walizo nazo ndugu wengine wengi hudumani, kama vile redio

na televisheni, na magazeti na kadhalika. Na kwa kufanya hivyo, mbona, mtu fulani angesema, "Ndugu Branham anapaswa kuwa hapa." Sasa nimetangazwa katika sehemu tatu juma hili, leo tu, sehemu tatu mbalimbali. Moja huko chini Kentucky, mbili huko California, niijuayo. Wala hakuna unachoweza kufanya juu yake, kwa sababu sina njia nyingine rasmi ya kutangazia, kwa hivyo inalifanya gumu.

7 Na, naam, ikitokea kuwa kuna mtu kutoka huko chini karibu na Madisonville, Kentucky, hapa. Nilitangazwa kuwa huko chini wiki iliyopita, wala sikujua chochote kulihusu. Nami nikaja nyumbani, na—nao walikuwa wamelitangaza; naye ndugu aliyefanya hivyo, jina lake ni Epply. Ama, naamini hilo lilikuwa jina lake. Kwa nia njema kabisa, alifanya hivyo. Alinipigia simu na kuniuliza ikiwa tunaweza kushuka tu tupate ku—kuwa baraka na kupata baraka kutoka kwa watu wake. Naye akapiga simu. Nikamwambia amwulize Ndugu Moore. Vema, basi, ilibidi niondoke. Nikamwambia ilinibidi kuondoka siku iyo hiyo. Vema, Ndugu Moore alishindwa kumjulisha mtu yeyote. Ndipo wakati, ama kunijulisha, ama kumjulisha mke wangu. Kwa hiyo nilikuwa huko Idaho, na nilikuwa tu nimerudi, nao mkutano ulikuwa unaendelea.

8 Kwa hiyo, na kwa hiyo niliona, kwenye wakati huo, haiwezi kufanya maandalizi huko Louisiana kwa mambo yanayoendelea hapa. Kwa hiyo, nilichukua tu maandalizi hayo mimi mwenyewe, kujifanyia maadalizi yangu kwa ajili ya hiyo mikutano, mpaka mikutano yangu imeninii...Kidogo nilininii...Loo, sijui, nadhani maungamo ni mazuri kwa nafsi. Hamfikirii hivyo? Nimezembea sana kuhusu mambo haya. Na kumruhusu mtu yeyote, popote pale, naliachilia tu bila mpangilio. Nami nimegundua, halifai kitu. Baada ya muda mrefu, unaweka... Inakubidi kuwa na mfumo fulani kwake. Na sasa ninajaribu kufanya maandalizi.

9 Nami—nami nitaenda kumwona Bibi Arnold. Mimi...Kuna mtu hapa Louisville ambaye amekuwa mzuri sana, nilipokuwa na mikutano hapa, na jina lake ni Ndugu Burgum. Naye alitaka u—usiku mmoja au mbili, ibada. Ninaenda kumwona maskini Teddy wake, naamini, Teddy Arnold. Kwa muda fulani wiki hii.

10 Ndipo Jumamosi na Jumapili ijayo, nikiweza, Bwana akipenda, ninataka kuwa huko chini Madisonville. Walikuwa na wahudumu ishirini na watano, thelathini huko nje. Wote wameketi pale, wakaja kwa ajili ya baadhi...Mmoja alikuwa maili mia sita, saba. Vema, hakuna mtu huko, kwa hivyo hakuwepo, wala si kosa langu mwenyewe, lakini nilininii tu... lakini kwa kuelewa vibaya tu, au kupuuza kumwita. Nami nitajaribu kuwa kule chini wikendi ijayo, Bwana akipenda.

11 Kisha, tarehe tano hadi sita, nitakuwa Brooklyn, New York. Na kisha kuanzia hapo, tarehe kumi na nne, kumi na tano, na

kumi na sita, huko Parkersburg, Virginia Magharibi. Nimefanya tu maandalizi hayo mawili jana usiku na asubuhi ya leo. Sasa, Charlotte, Carolina Kusini, iko tu kwenye orodha, lakini sijui. Halafu, likizo inakuja.

12 Ndipo tutaenda kwenye Pwani ya Magharibi, ambako wanaandaa m—mkutano mkubwa kwenye ukumbi. Sasa, hii ni—ni mikutano midogo sawasawa na ya shule za upili na vitu kama hivyo. Ule wa huko Pwani ya Magharibi, utakuwa wa mi—miji miwili, mkutano wa pamoja wa jiji, wa Oakland na San Francisco.

13 Na halafu wajumbe wa Phoenix, kwa kuwa Ndugu Roberts hawezi kuwa kule mwaka huu, kwa namna fulani ninapaswa kupachukua mahali pake kule Phoenix, katika—katika mkutano wa mkoa mzima wa Marikopa. Hiyo ni juhudi ya muungano.

14 Basi mniombee kwa sababu na—nayahitaji. Nami ninatambua kwamba kila wakati imani inapojiweka yenyewe, ibilisi anaelekeza kila bunduki katika kuzimu juu yake, namna hiyo, mnaona, kwa hiyo inaifanya kuwa ngumu sana.

15 Kwa hiyo, asubuhi ya leo, kuwaombea wagonjwa. Ninataka kusoma baadhi ya Neno la Milele la Mungu, na kuongea kwa dakika chache tu kutoka kwenye Maandiko, na kisha kuwaombea wagonjwa. Loo, jinsi ninavyopenda kuongea juu Yake! Nanyi je? Ninapenda tu kuongea juu Yake.

16 Sasa nataka kusoma kutoka katika Biblia, Wafalme wa Pili mlango wa pili, kifungu cha 12, sehemu yake.

> *Naye* Eliya *akaona, na*. . .*akalia, Baba yangu, baba yangu,* magari *ya Israeli, na wapanda farasi wake.*

17 Na sasa kwa njia ya fu—fungu la maneno ama somo, nataka kuzungumza juu ya: *Joho La Kuachiwa*. Kwa hiyo Bwana na aongeze baraka Zake tunapozungumza nanyi asubuhi ya leo. Nanyi mwe mkituombea.

18 Mnamo wakati huu wa utawala wa Israeli katika hiyo nchi. Israeli ilikuwa taifa, nayo ilikuwa taifa lenye nguvu, na kidogo ulikuwa wakati wa amani miongoni mwa sehemu yake ya kijeshi. Lakini katika se—sehemu yake ya kiroho, kidogo ilikuwa ni wa—wakati wa—wa uigaji. Na tukitazama nyuma katika Agano la Kale, kila mara tunaweza kupata mifano ya kile kinachoendelea siku hizi. Kila mara, katika Biblia, mambo yaliyopo sasa, ni mifano tu ya yale yaliyokuwa hapo mwanzoni.

19 Sasa, Kitabu cha Mwanzo kinatoa kila kitu kilicho ulimwenguni leo. Hakuna kitu ulimwenguni ila ambacho hakikuanza katika Mwanzo, kwa maana huo ndio mwanzo. Hapo ndani, kila itikadi ilianza. Katika Mwanzo, kulianza kila kitu kilichoanza. Nalo Kanisa la kweli lilianza katika Mwanzo. Na mwaminio bandia alianza katika Mwanzo. Na kutojali kulianza katika Mwanzo. Mwanzo kilikuwa ndicho chimbuko.

20 Na sasa wakati wa utawala wa Eliya, au safari ya Eliya hapa duniani, ambaye alikuwa nabii wa Mungu kwa wakati huo.

21 Naye Mungu hajawahi kujiacha Mwenyewe duniani bila shahidi. Mungu sikuzote, mahali fulani, sehemu fulani, amekuwa na mtu ambaye angeweza kuweka mikono Yake juu yake na angesimama kama shahidi. Kwa hiyo kama Yeye amefanya hivyo, huko chini tangu Mwanzo, mwanzoni, hakika, mahali fulani, Mungu ana mtu ambaye anaweza kumwekea mkono Wake sasa. Kwa kuwa Yeye—Yeye ni zaidi ya mtu mmoja sasa, anao watu wengi anaoweza kuweka mkono Wake juu yao, kwa sababu tunashuka kwenye wa—wakati wa kukusanya, wakati wa mavuno.

22 Mwanzo kilikuwa ni kupandwa kwa mbegu, nayo hii miaka elfu sita imekuwa ni kule kukomaa kwa mavuno. Na sasa mbegu imekuwa mbegu yenyewe. Imerudi kwenye kuchanua, na kutoka kuchanua hadi kwenye—kwenye tunda. Na ni wakati wa kukusanya sasa, wakati wa mavuno, mambo yote makuu yaliyoanza. Kanisa la kweli lililoanza katika Mwanzo limefika kwenye wakati wa tunda, tunda la Roho. Naye mpinga-Kristo aliyeanza katika Mwanzo amefikia kwenye tunda lake. Nasi tuko katika wakati wa kumalizia wa kipindi kizima cha wakati cha ulimwengu, ninii . . . cha mwanadamu. Nasi tunaninii . . . Ndio wakati mkuu sana ambao mtu yeyote, ama kwenye wakati wowote, amewahi kuishi, ni wakati huu. Ni wakati wa kutetemeka. Ni wakati wa shida kwa wenye dhambi, lakini ni wakati mzuri sana kwa Wakristo, kwa sababu tunajua kwamba tu—tunafunga virago, ama kuunganisha pamoja juhudi ndogo za mwisho, kwenda Nyumbani na kumlaki Bwana.

23 Sasa watu, siku hizi, mnapotazama kote na kuona taabu na dhiki kuu inayolikabili taifa, ambapo . . . Siku chache zilizopita usiku, nilikuwa nikizungumza na mtu fulani, alikuwa mmoja wa mawakala hawa hapa waangalizi wanaolinda, nao wakasema, "Ndugu Branham, tuliagizwa tu na serikali kamwe tusiwashauri watu tena kulala chini karibu na . . . mbali na dirisha sakafuni, kama bomu likipiga, au kamwe wasiingie kwenye ghorofa ya chini, kwa sababu bomu hili jipya ambalo wangeweza kuliongoza kwa redio kutoka Moscow hadi Barabara ya Nne ya Louisville, na kulipukia moja kwa moja barabarani, walirushe, ina ninii . . . vitu ndani yake, baruti kali, na kuvirusha maelfu *kadhaa*, maelfu *kadhaa*, likiongozwa na nyota na rada, na kuliangusha papo hapo kwenye Barabara ya Nne Louisville, kutoka Moscow, Urusi, na litakapofika pale, si lazima litumie ndege wala chochote, ni kulirushia tu *hapa*, nalo litaanguka tu papa *hapa*, nalo litachimba shimo ardhini, kwenye eneo fulani, kina cha futi mia moja na sabini na tano kwa maili kumi na tano mraba ama popote liendapo, maili kumi na tano mraba." Hakuna la kufanya ila kujiandaa kupanda kwenda juu, ndilo jambo pekee la kufanya nyakati hizo zifikapo.

24 Hebu wazieni tu, wanaweza kurusha hayo hamsini, ama mia moja, kwa wakati mmoja, kama wangetaka kurusha. Yote yatakwisha, katika kipindi cha. . .Ninaamini ni dakika sitini ama themanini, ama chochote kile, au sekunde—sekunde, hasa, kutoka kule mpaka hapa, kufikia maangamizi yote ya kitu hicho chote kutukia. Hakutakuwa na chochote kitakachosalia kati ya Louisville na Henryville, na kati ya Louisville na—na Bardstown, ama kule chini, ila shimo moja ardhini pamoja na lundo la mavumbi ndani yake. Hilo tu ndilo lingesalia, mbali na maeneo ambayo lingefikia, na kuchoma moto kwa maili na maili na maili mbele yake. Na wakati moja linaanguka kule, lingine linaanguka mahali pengine, likakutane nalo.

25 Nina furaha sana kuwa tunalo Kimbilio la kujisetiri. "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia wakawa salama." Haijalishi ni mabomu mangapi au ni kiasi gani cha kitu kingine chochote. . .Tuko salama Huko. Kwa hiyo, ulimwengu na mwenye dhambi, kwa kuwa hawana Kimbilio hili, ama Mahali hapa pa usalama, ni wakati wa kutetemeka. Ninaamini, kama nisingalikuwa Mkristo, ningeingia wazimu, nikiwazia kile ambacho kinaweza kutokea wakati wowote. Na nikiwa na nyumba iliyojaa watoto wadogo, na kila kitu, nisingejua la kufanya. Lakini nina furaha sana kwamba ninaweza kusimama nyumbani kwangu na kuwaonyesha Makao ambayo hakuna bomu linaloweza kugusa, wala kitu kingine chochote, chini ya Mabawa ya ulinzi ya Bwana Yesu. "Si kwa nguvu, si kwa uwezo, bali ni kwa Roho Yangu," asema Bwana. Mnaona? Huo ndio ulinzi wetu.

26 Na ni wakati mkuu na mtukufu jinsi gani, kujua kwamba dhambi na harakati zote na majaribu ya maisha yatakwisha hivi karibuni. Yote yatakwisha moja ya siku hizi, nasi tutaenda Nyumbani kuwa pamoja na Bwana. Sasa, kilichosalia ni wakati wa kuihubiri Injili na kuwaleta wengi, wengi kadiri tuwezao kwenye Mnara huu mkubwa.

27 Na halafu, tunapoona mfano wa somo letu leo hii, la Eliya, wakati wa utawala wake, yeye. . .ama, safari yake ya duniani, mbona, alikuwa mtu mkuu, mwenye nguvu. Mungu alikuwa akimtumia kwa njia kuu, kwa uwezo mkuu. Nasi tunaona ya kwamba mnamo wakati huu, kulikuwako na kundi la waigaji waliojaribu kumwiga Eliya, ambao walijaribu kufanya mambo yale yale aliyofanya Eliya.

28 Na kwa hiyo tunaona jambo lilo hilo siku hizi; uigaji wa Ukristo, watu wanaojaribu kutenda kama Wakristo, wanaojaribu kujifanya Wakristo. Huwezi kufanya hivyo. Mungu hana budi kufanya hivyo. Yeye Ndiye pekee awezaye kufanya hivyo.

29 Kwa hiyo walianzisha shule, nao wakaiita, "shule ya manabii." Nao wote wakaenda kwenye hiyo shule ya manabii,

nao wakawaelimisha. Nami naweza kuwazia wahubiri hao wote kule juu, wamevaa joho kama aina ile ile alilovaa Eliya. Ninaweza kuwazia wakijaribu kuiiga sauti yake, jinsi alivyoongea. Na—na jinsi alivyoonekana, kila mtu akijaribu kufanya jambo lile lile, kwa maana Eliya alikuwa mtu mashuhuri aliyetumiwa na Mungu.

30 Na tunapata jambo lile lile siku hizi. Nilikuwa nikisikiliza matangazo ya redio, si muda mrefu uliopita. Wana Billy Graham wengi kote nchini, tangu Billy alipokuwa Louisville. Kila mtu akijaribu kuiga kitu kile kile, karibu wanachanua nywele zao vile vile, na—na kuvaa kitu kile kile, na sauti ya namna ile ile, na kadhalika. Lakini huwezi kufanya hivyo. Huna budi kuwa tu vile ulivyo na vile Mungu alivyokuumba. Hiyo ni kweli. Na kwa hiyo tunaona jinsi ambavyo, pengine, katika siku hizo jambo lile lile lilitukia.

31 Sasa, Mungu, akiona, akiona kimbele ya kwamba siku za Eliya zilikuwa zimehesabiwa, kwamba alikuwa na muda fulani angeweza kukaa hapa duniani, kama kila mtu alivyo nao. Kwa hiyo, alikuwa awe na mrithi wa Eliya. Basi alipomhitaji, Mungu alimwita mtu huyu. Hakuwa katika seminari yoyote alipomwita. Alikuwa akilima shambani, kwa nira ya maksai, akitumika, au akiwatunza mama na baba yake. Ndipo Mungu akamwita awe ndiye mrithi wa Elisha, ama Eliya.

32 Labda wengi kule shuleni walifikiri walikuwa na uhakika walikuwa wanaenda kuwa mrithi wake, walikuwa wanaenda kuvaa joho lake mara tu atakapomaliza nalo.

33 Lakini, Mungu ndiye aitaye. Mungu ndiye achaguaye. Mungu ndiye anayeteua. Mungu ndiye anayeweka katika utaratibu. "Mungu ameweka Kanisani: wengine, mitume; wengine, manabii; wengine, waalimu; wengine, wainjilisti; na wachungaji." Mungu hufanya hivyo, Mwenyewe. Hatuwezi kufanya unywele mmoja kuwa mweusi au mweupe, wala hatuwezi kujiongeza kitu kimoja kwenye kimo chetu kwa kujisumbua. Mungu, katika neema Yake isiyo na kikomo, na kwa uteuzi Wake na kujua Kwake tangu zamani, huweka mambo haya katika utaratibu, na kila gurudumu hufanya kazi sawasawa kabisa. Napenda hilo.

34 Ningekuwa mtu aliyevunjika moyo, asubuhi ya leo, kama sikuamini katika uteuzi na wito wa Mungu. Kama nilidhani ya kuwa ulimwengu huu uliachiwa matokeo yake, kwa uwezo wa mwanadamu, na kwa hekima ya mwanadamu, na kwa wale "mabingwa wanne," na ma-U.N., na ambao hata hawalitaji Jina la Mungu, ningekuwa mtu aliyeshushwa moyo. Bali siwategemei hao kwa matokeo yake.

35 Ninatazama chini katika kurasa za Kitabu hiki cha kale *hapa,* ambapo Mungu aliliandika, na kila kitu kitakuja jinsi tu hasa Yeye alivyosema, na hilo latosha. Kwa hiyo, jambo pekee

linipasalo kufanya sio kuwafuata, bali kuifuata Kalvari. Mfuate Mungu, lifuate Neno Lake, kaa katika Neno Lake. Haidhuru ni jinsi gani inaonekana itakuwa *hivyo*; itakuwa jinsi Mungu anavyokusudia iwe. Haiwezi kuwa kitu kingine chochote. Kwa maana, Yeye akiwa hana kikomo, alijua mwisho tangu mwanzo, Naye hufanya kila kitu kififikie sifa Zake. Hiyo ni kweli.

36 "Mambo yote yatalazimika kufanya kazi pamoja." Kila kitu kitalazimika kuumbika kupafikia mahali pake. Jamani! Ikiwa hilo lisingemfanya Mkristo awe na ujasiri! Hakuna kinachoweza kwenda mrama. Hata hivyo, si vita vyetu; ni Vyake. Si hekima yetu; ni Yake. Jambo moja pekee tulilopaswa kufanya ni kuweka imani na tumaini letu pale, na kutulia na kuuona utukufu wa Mungu, tuone jinsi linavyozunguka mpaka mahali Pake, na kila gurudumu likisonga. Huenda likatapakaa huku na huko, lakini litasonga mbele moja kwa moja hadi mahali Pake panapofaa wakati Mungu anaponena Neno.

37 Alijua mwisho tangu mwanzo. Alijua alikuwa anaenda kuchagua. Alijua Elisha angepachukua mahali pa Eliya, kabla ulimwengu haujaumbwa. Kila kitu hakina budi kufanya kazi sawasawa kabisa.

38 Nasi tunawahofia wapendwa wetu, na kadhalika, "Je, watawahi kuingia?" Majina yao, kama yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, watafanya kazi moja kwa moja humo ndani. Hilo ndilo jambo pekee analoweza kufanya. Tunatoa ushuhuda na kuiangaza Nuru. Mungu hufanya hivyo, Yule anayewaletea.

39 Sasa angalia, katika Eliya, basi, baada ya kumtupia joho lake, na kujaribu kumvisha. Kwa maneno mengine, Eliya nabii, ambaye alikuwa na vazi la Mungu mabegani mwake, alishuka na kuliweka juu ya Elisha, mkulima, aone kama lingemtosha. Ndipo ikachukua kama miaka kumi kubadilishwa, vazi hilo lipate kumwenea.

40 Unajua, kwa kawaida Mungu hutuweka kwenye karakana na kutuchonga. Sasa, Yeye hakubadilisha vazi lake limtoshee Elisha; alimwamuru Elisha aenee kwenye hilo vazi. Na hivyo ndivyo afanyavyo siku hizi. Yeye hutubadilisha tupate kutoshea kwenye vazi, si vazi litutoshee. Wakati mwingine tunataka kufanya vazi litutoshee, lakini hatuwezi kufanya hivyo. Inakubidi (kuacha) ubadilishwe, wewe mwenyewe, kwa ajili ya vazi. Ni vazi la Mungu, Naye alilifanya kamilifu. Nasi tunapaswa . . . Hana budi kutuingiza katika milki hiyo, kufanya vazi litutoshee.

41 Kwa hiyo, hatuwezi kuwa wakamilifu, sisi wenyewe. Tunajua hatuwezi. Hakuna njia ya sisi kuwa, na, hata hivyo, Yeye alisema tuwe. Kwa hiyo, lakini, kile alichofanya, Yeye alifanya upatanisho kwa ajili yetu; Bwana Yesu Kristo na haki Yake.

Hapo ndipo ukamilifu unakuja; kwa kupuuza utakatifu wetu wenyewe, ambao hatuna wowote; na mawazo yetu wenyewe, ambayo hayapaswi kuwapo. Lakini tunatulia kwa dhati juu ya kazi iliyokamilika ya Bwana Yesu. Mungu alimtuma duniani, na ni ndani Yake tunatulia.

42 Angalia, miaka hii yote, tujuavyo sisi, yeye alipitishiwa tu ubatizo huo mmoja wa joho juu yake. Lakini kote katika miaka, Mungu alikuwa ameifinyanga tabia ya huyo mtu kufikia mahali ambapo, baada ya wito wake, kwamba angeweza kutoshea katika vazi hilo na kuwa mtumishi wa Bwana.

43 Ndipo basi Eliya alipopitia hapo na kumtupia hilo, nao wakaelekea Gilgali na sehemu zingine nyingi walizopitia, hata kwenye shule ya manabii, wakienda zao, wakiendelea na safari. Na, hatimaye, Eliya alikuwa akijaribu kumfanya Elisha arudi. Je, mliliona? Kujaribu kumfanya arudi. Kasema, "Mimi . . ." Vinginevyo, "Labda barabara kidogo ina mwinuko mkubwa sana kwako, mwanangu. Labda ni nyembamba sana kwako kutembea."

44 Mnajua, mahali Eliya alipokuwa, palikuwa ni unyofu. Na popote mtumishi wa kweli wa Mungu anapoihubiri Injili, ni Injili iliyonyooka, isiyoghoshiwa ambapo inahubiriwa.

45 Mbona, siku moja, alienda kule kwenye shule ya manabii, kuwatembelea, nao wakamwomba aondoke. Walisema, "Imenyooka kupita kiasi hapa, kwetu sisi."

46 Tunachohitaji leo hii ni mahubiri ya Injili, yaliyonyooka zaidi ambayo yatatenganisha ngano na makapi, ama mema kutoka kwa mabaya. Yafanye kilicho cha kweli ni "kweli," na kilicho cha uongo ni "uongo."

47 Watu hawa wote pamoja na ujuzi wao, na yote waliyokuwa! Wakatuma watu kutafuta chakula, na mmoja wao akachuma mzabibu mwitu, na akachuma matango mwitu, ndipo akapika mauti katika sufuria yao ya kikanisa. Na, muda si muda mwajua, walilia kwa sauti kuu, "Mauti imo sufuriani!"

48 Lakini Eliya, akiwa na sehemu maradufu, alijua la kufanya, kwa hiyo akatia konzi ya unga sufuriani. Kasema, "Haya kuleni." Kwa maneno mengine, wao . . .

49 Leo hii, mfano fulani, ningefikiri, ya kwamba tuna Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Walutheri, Wapentekoste wengi, na chochote kile, yote yamechanganyikana, na mmoja akimshambulia mwenzake. Wala hatuna haja ya kukiondosha kitu hicho chote na kukiondolea mbali. Tunahitaji konzi nyingine ya Unga. Dumisha kanisa lile lile.

50 Huo unga ulitoka kwenye nyumba ya hiyo shule pale, ambao ulikuwa ni unga wa sadaka ambao watu walikuwa wameleta, na malimbuko ya mavuno yaliyosagwa kwa kinoo fulani kilichofanya kila nafaka kuwa sawa. Halafu basi wakati . . .

51 Unga huu, ukiwa ni uleule, ulikuwa ni mfano wa Kristo. Unga ni uhai. Na wakati mfano wa Kristo, ule unga, ukisagwa vivyo hivyo; unamaanisha, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele." Nao ule unga katika sadaka ya unga, na walipouweka unga huu mle ndani, kumtia Kristo mautini kulileta Uzima. Hilo ndilo linaloleta tofauti katika hali yetu iliyokufa, katika tofauti zetu, katika mabishano yetu ya kikanisa na kila kitu. Kama tungemwingiza tu Kristo ndani yake, ingebadilisha mauti, na utengano, kuwa Uzima, kama tu tungelifanya hivyo.

52 Kuna Wabaptisti milioni kumi na tisa Marekani. Kuna Wamethodisti milioni kumi na tatu Marekani. Kuna Walutheri milioni kumi na moja Marekani. Na Wapresbiteri milioni kumi Marekani. Na Mungu pekee anajua ni Wakatoliki wangapi, ambao wanashinda kwa wingi lolote la hayo madhehebu. Lakini, katika hayo yote, tunahitaji nini? Unga kidogo. Tunahitaji kuleta Uzima kanisani. Naye Kristo ndiye Uzima. Alikuja kutuletea Uzima.

53 Kwa hiyo, walikuwa na ugomvi wao, na shule zao, na theo-. . . theolojia zao, na kadhalika.

54 Ndipo Eliya akamwambia Elisha, "Afadhali urudi, kwa sababu njia inaweza kuwa ngumu kidogo." Lakini mtu wa Mungu ambaye wakati mmoja amekabiliana nayo, ama ametupiwa begani mwake vazi la haki na uweza wa Mungu, si rahisi sana kurudi nyuma.

55 Nilipomsikia mchungaji akisema, asubuhi ya leo, kwamba nanii wetu. . . "Wengi wanakufa moyo." Tunachohitaji, ndugu, ni kuwa na ujasiri! Tunachohitaji ni kutiwa moyo, hiyo ni kweli. Majaribu yanaweza kuja. Kamwe hatukuahidiwa kuwa huru nayo, lakini Yeye atatupa neema ya kuyavuka. Ikiwa mlima ni mrefu sana huwezi kuupita juu, una kilindi sana huwezi kupitia chini yake, ni mpana sana usingeweza kuuzunguka, Yeye atakupa neema ya kuuvuka. Hiyo ni kweli. Usiwe na wasiwasi, bali mtazame Kristo, kwa maana Yeye Ndiye pekee awezaye kutuvusha.

56 Sasa, tunawaona wakiendelea na safari, kuja shuleni. Naye akasema, "Kaa hapa sasa. Kuwa hapa, na utulie uwe mwalimu mzuri wa theolojia, na kadhalika. Na pengine, siku moja, unaweza kuwa mkuu wa chuo hapa. Lakini sina budi kushuka kwenda mbele kidogo."

57 Unaweza kumwazia mtu wa Mungu akiridhika kuwa mkuu wa chuo, wakati Nguvu za Mungu zikiwa pale pale alipokuwa amesimama? La, bwana. Akasema, "Kama Bwana aishivyo na roho yako iishivyo, sitakuacha." Napenda hilo.

58 Kaa nalo, haidhuru umeshushwa moyo kiasi gani, hata kama inatoka kwa mama yako, baba yako, au kutoka kwa mchungaji wako. Kaa Naye.

59 Hao wakaenda mpaka Yordani. Wakavuka. Ndipo Eliya akasema, "Sasa ungetaka nikufanyie nini?"

60 Akasema, "Sehemu maradufu ya roho yako na ije juu yangu." Alijua alikuwa na kazi ya kufanya. Akasema, "Sehemu maradufu." Sio tu tukio zuri motomoto, sio tu kupeana mikono kuzuri, au ushirika mzuri na watu wengine wa kanisa. Lakini, "Ninachohitaji ni sehemu maradufu ya kile kilicho bora zaidi sasa."

61 Ninawaambia, Mungu anapomweka mtu kwa ajili ya kazi ya ulimwengu, hana budi kuwa na kitu bora kuliko ulimwengu ulicho nacho. Hana budi kuwa na kitu bora kuliko kanisa lilicho nacho. Hana budi kuendea cha maradufu.

62 Na kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo sehemu maradufu ilihitajika, ni leo hii, katika milki za watu; kitu bora zaidi, kitu cha juu zaidi. Siwezi. . .Nadhani maharagwe na ugali wa mahindi ni mazuri sana, lakini wakati mwingine sina budi kupanda juu zaidi kidogo. Nasi hufanya hivyo; hatuna budi kufanya. Inabidi tuendelee kupanda. Israeli walikuwa wakirudi nyuma kama waliendelea kukaa mahali pale pale. Inabidi awe anaendelea mbele au kurudi nyuma. Na hivyo ndivyo kanisa lilivyo.

63 Kwa hiyo, walipokuwa wakienda mbele, haikupita ila dakika chache mpaka akasema, "Umeuliza jambo kubwa, lakini, hata hivyo, ukiniona nitakapoondoka, unaweza kupata ulichoomba."

64 Sasa, hiyo haina budi kuwa umoja wa nia, umoja wa moyo, mtazamo mmoja, ukilielekeza jicho lako kwenye ahadi. Hum! Kama wewe ni mgonjwa asubuhi ya leo, kama unateseka, kuna ahadi moja kuu; si ya Eliya, bali ya Mungu Mwenyewe. "Kama unaweza kuamini, unapoomba, amini kwamba umepata kile unachoomba, nawe utakipokea." Haijalishi daktari anasema nini, ni kiasi gani *hiki* kinakwenda au *kile* kinakwenda; shikilia ahadi kwa dhati.

65 Eliya alimpa agizo, "Ukiniona ninapoenda, itakuja juu yako."

66 Hiyo hapo ahadi, "Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana kwa hao waaminio."

67 Wakati mwingine ninajiangalia na kuwazia, "Nimekuwa yavuyavu sana maishani mwangu. Nimengoja, na kukosa maelfu mengi ya watu, kuwaingiza katika Ufalme, kwa sababu nimengoja na kusema, 'Mungu. . .' Nikaitegemea sana karama ya kiroho. Na kusema, 'Bwana, laiti ungalinionyesha, laiti ungalinipa ono la jambo ninalopaswa kufanya.'" Naye Mungu anatoa ono, kisha nitageuka na kumwacha mtu fulani anizungumzie jambo lingine.

68 Na, loo, sijawahi kupafikia mahali hapo, bado, mpaka mimi. . .kama nilivyofanya wakati huu, ambapo ninahisi ni

imani, ambapo hatuna budi kwenda huko nje, kwa kuwa ni ahadi. Na mambo ambayo amefanya, na uponyaji aliofanya, na miujiza; kiasi kwamba, ameshuka na kupigwa picha Yake kando yetu, na kadhalika, ambalo halijawahi kujulikana tangu ulimwengu uanze. Halafu ati kusimama kama yavuyavu? Hata inanifanya mwenyewe kupoteza matumaini. Ni wakati wa kuweka macho yako kwenye ahadi.

69 Na hivyo ndivyo, kwa neema ya Mungu, ninalenga kufanya. Nami ninatambua ya kwamba kila ibilisi wa kuzimu atalitupia risasi. Lakini, kwa neema ya Mungu, ninakusudia kuweka jicho langu kwenye ahadi.

70 Elisha akasema, "Ikiwa wewe," au, Eliya akasema, "Ukiniona wakati nikiondoka, utapata kile ulichoomba." Hiyo ni kweli. Huna budi kuweka jicho lako juu yake; uiangalie ile ahadi. Kama vile, vipi kama baadhi ya shule, akigeuka, na kusema: "Hei, jamani, ninaendeleaje sasa, nikifuata moja kwa moja nyuma ya nabii?" Angeshindwa, labda. Lakini hakujali shule ilichowazia, au waalimu wote walichowazia. Hakujali majirani waliwazia nini, au hizo nyumba, au ni nani aliyemtazama. Aliweka imani yake katika ile ahadi.

71 Tunachohitaji leo ni imani katika ahadi ya Mungu, wala usizingatie anachosema *huyu* au anachosema *yule*.

72 Kama vile ndugu mmoja alivyosema, mhudumu mmoja alikuwa na wasichana wawili ambao walikuwa bubu, na kwamba ukosoaji juu ya uponyaji wa Kiungu, kwamba, "Watoto hao hawangeweza kuponywa."

73 Usisikilize wakosoaji. Weka imani yako juu ya ahadi. Mungu alisema hivyo! "Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, naye Mungu atawainua." Kama anaweza kumfanya kiziwibubu mmoja kusikia, basi anaweza kumfanya kiziwibubu mwingine kusikia. Tunajua, kwa uthibitisho usiokosea, ya kwamba Yeye hufanya hivyo. Tuidumishe imani yetu juu ya ahadi. Macho yetu moja; masikio yetu moja; mioyo yetu moja; na, jambo moja, juu ya Yesu Kristo, Naye anaweza kutimiza yale aliyoahidi. Loo, tunapowazia jambo hilo, inabadilisha mandhari yote tunapopata hilo. Mungu alitoa ahadi. Mungu ndiye aliyesema hilo.

74 Sasa, *hapa* alikuwapo mwakilishi wa Mungu alisema jambo hilo, na sasa Mungu Mwenyewe amelisema. Basi tufanye nini? Hakuna kitu ila kuweka mawazo yetu juu ya hilo. Kasema, "Ukiniona ninapoondoka, unaweza kupata hiyo ahadi." Elisha akamkazia macho Eliya. Haijalishi ni nini kilichofoka maneno kutoka kila upande, kile kilichotukia kila upande, kile kilichotukia kabla ya hapo, yeye hata hakukitazama. Alielekeza macho yake kwenye ile ahadi. Haya basi, macho yako kwenye ahadi.

75 Ninawaza juu ya yule mama tuliyemtembelea hivi majuzi usiku, Dada Sauer. Huku daktari akimwambia jinsi alivyokuwa katika hali mbaya. Nami sikumwambia; nilimwambia mpendwa wake. Na jinsi isingewezekana kwake kupata afya. Sasa, ndugu, mkwe wake aliniuliza kuhusu hilo. Nikasema, "Laiti angaliyaelekeza macho yake kwenye ahadi." Haijalishi ni nini kitakachotukia, weka macho yako kwenye ahadi.

76 Wiki chache zilizopita, Dada Wood hapa, na Ndugu Wood, marafiki zetu wawili wa karibu hapa kanisani. Nilikuwa Michigan na marafiki zangu, Leo na Gene. Tulikuwa tumetoka kwenye mkutano wa Chicago na kwenda na baadhi ya watu wao, kwa . . . kwa siku mbili, kwenda kuwinda kulungu kwa pinde na mishale. Basi nilipokuwa njiani nikirudi, mke wangu alikuwa amenipata, naye akasema, "Mwombee mama yake Bibi Wood. Kansa inaula uso wake." Kisha kasema, "Sijapata kumwona Dada Wood akifadhaika hivyo. Analia." Dada Wood sikuzote amekuwa shujaa wa imani, tangu Mungu alipomponya mvulana wake mguu uliolemaa, na kumponya yeye TB, na kadhalika. Lakini alikuwa dhaifu.

77 Pale chumbani, usiku huo, tuliomba. Tukiingia, Bibi Wood alisema, "Ndugu Branham, tutaenda kule." Basi tukaenda kwa mama yake, aliyekuwa Louisville. Naye alikuwa na kansa kando ya pua yake, naye daktari alikuwa ameigusagusa, akaitawanya; mpaka ikawa ni duara ndogo tu kando ya pua yake, na juu tu kama moja juu ya nane ya inchi kutoka kwenye jicho lake, mfupa tu uliokaa pale. Imeila tu upesi ilivyoweza kuila.

78 Nikaingia chumbani, nikapiga magoti. Nikasema, "Nataka kuzungumza naye peke yangu." Nami nikaingia chumbani kuomba pamoja na huyo mwanamke. Basi nikiwa humo chumbani, nikawazia, "Ee Mungu, laiti ungenionyesha ono la kile kitakachompata huyu mwanamke." Bw. na Bibi Wood wameketi nje, wakingojea kuona kile ono lingesema.

79 Lakini nilipokuwa huko, nilihukumika. Nilihukumika kwa kungojea ono. Ilionekana kama kitu Fulani kilirejea nyuma, "Haikuwa wito. Unahitaji ono la nini, wakati ahadi tayari imeshasemwa?" Kwa hiyo nikapiga magoti na kuomba. Na wakati nikiomba, kitu fulani kikatia nanga ndani, imani ya ile ahadi.

80 Nikarudi nje. Naye Bibi Wood, nilipomwambia kuhusu jambo hilo, alisema, "Je, uliona chochote, Ndugu Branham?"

81 Nikasema, "Sijaona kitu hasa, lakini nilihisi kitu Fulani kilichoniambia kwamba ahadi Yake ilikuwa ni kweli na Yeye angeitimiza. Nami ninaamini ya kwamba atafanya hivyo."

82 Ndipo chini ya saa ishirini na nne, mwisho wa kansa hiyo ukaanza kusambaratika na kutokea upele juu yake. Kansa haitoi upele, kama mjuavyo, isipokuwa imekufa. Basi ndiyo hiyo sasa. Naye huyo mwanamke ameponywa, na yuko nyumbani. Ni

Kristo wa ajabu jinsi gani! Kwa kuweka macho yetu kwenye ahadi! Mungu alisema hivyo!

83 Lakini tunapoombewa, wakati mwingine, tunaenda kando na kusema, "Vema, haukufanyika mara moja, kwa hivyo labda afadhali turudi tena." Loo, la.

84 Weka macho yako kwenye ahadi. Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Ni hayo tu. Ikiwa Mungu alisema hivyo, Mungu anaweza kutimiza ahadi Yake, la sivyo hatawahi kuitimiza.

85 Ibrahimu aliviita vitu hivyo ambavyo havikuwepo kana kwamba vilikuwapo. Na, kwa muda wa miaka ishirini na mitano, alisimama juu ya yasiyowezekana, kwa maana alihesabu kwamba Mungu aliweza kutimiza yale aliyoahidi. Amina. Nasi ni watoto wa Ibrahimu, kwa imani.

86 Bila shaka, Eliya aliweka macho yake juu ya . . . au Elisha juu ya Eliya, na walipokuwa wakiendelea mbele. Na baada ya kitambo kidogo, gari la farasi likaja na kuwatenganisha, mmoja upande mmoja na huyo mwingine upande mwingine, kisha likamchukua Eliya. Juu ya . . . Alipanda hilo gari la farasi, akapanda juu, kisha akalivua vazi lake begani mwake akamrushia Elisha. Kwa sababu, Elisha alikuwa amekulia ndani yake, mwajua, kwa hiyo likamtoshea sawasawa. Nanyi mngeweza kuwazia . . .

87 Loo, nataka mnipe usikivu wenu wote, ninapohisi koo langu likitekenya. Nataka kuwaulizeni jambo fulani.

88 Mnaweza kuwazia jinsi Elisha alivyojisikia alipoliokota vazi hili, akaliweka begani mwake mweyewe? Loo, ni hisia ya jinsi gani!

89 Simaanishi jambo hili kuwa la kibinafsi, lakini yapata miaka kumi iliyopita, kutoka mimbarani hapa, nilihubiri juu ya somo; Daudi, yule shujaa akiwa na kombeo mkononi mwake, na Goliathi mbele zake. Katika siku hizo hapakuwapo na miamsho ya uponyaji hudumani, popote, tuliyoijua. Na, loo, jinsi watu walivyoukosoa uponyaji wa Kiungu! Lakini kulikuwako na kitu fulani, baada ya kukutana na Kiumbe fulani. Nao wachungaji waliniambia kwamba nilikuwa ninarukwa na akili zangu, ya kwamba isingewezekana. Lakini, kutoka kwenye kisanduku kiki hiki hapa, nilizungumza juu ya Daudi. Kasema, "Je, mnataka kuniambia kwamba haya, majeshi ya Mungu aliye hai, yatamwacha yule Mfilisti asiyetahiriwa kulitukana jeshi hili?"

90 Maskini kijana mdogo mwenye mabega yaliyoinama, nywele za kipilipili na amevaa kanzu ya ngozi ya kondoo, na kombeo mkononi mwake; huku jeshi zima la Israeli limerudi nyuma, likasimama. Naye, peke yake, akajitokeza. Pamoja na mtu, aliye na—aliye na mkuki wenye urefu wa futi kumi na tisa, na kitu kilichokuwa nchani mwake kilikuwa na uzito wa shekeli kadhaa, labda ni ratili ishirini za chuma, umenolewa, mkuki wa futi kumi na tisa, akiwa na vidole vyenye urefu wa inchi kumi na nne.

Na huenda Daudi alikuwa na uzito wa ratili tisini, ndipo akasimama, akiruka-ruka, kama jogoo mdogo, huku akisema, "Mnataka kuniambia," loo, jamani, "kwamba mtamruhusu Mfilisti huyo asiyetahiriwa! Akikaa mahali pake, basi akae, lakini anatukana majeshi ya Mungu aliye hai." Loo, jamani, ni shujaa wa jinsi gani! "Na nyinyi nyote mnaogopa kwenda kupigana naye?" Kasema, "Acha nikabiliane naye." Loo, jamani! Akasema, "Mungu wa Mbinguni alinijalia kumwua simba kwa kombeo, alinijalia kumwua dubu kwa kombeo, basi ni zaidi sana jinsi gani atamtia Mfilisti huyo asiyetahiriwa mkononi mwangu!" Hakika.

91 Basi ushindi wa kwanza ulipopatikana, naye Goliathi amebwagwa chini, majeshi yote ya Israeli yakamfuata Daudi. Nao wakakata vichwa na kuwapiga, Israeli. . .au kuwapiga Wafilisti mpaka ndani ya nchi yao wenyewe. Waliwafinyilia pembeni, na kuwachinja, na kuiteka miji yao, na kila kitu, nao wakapata ushindi.

92 Ndugu na dada, jambo lile lile limefanywa katika milki za mambo ya kimbinguni, waliposema, "Uponyaji wa Kiungu hauwezi kufanya kazi. Siku za miujiza zimepita." Ikiwa siku za miujiza zimepita, siku za Mungu zimepita. Kanisa ambalo haliamini katika mambo ya kimbinguni hatimaye litakufa, naye Mungu ataachana na hilo kanisa. Lazima! Naye Mungu alitoa ahadi, nazo ahadi za Mungu ni za Milele.

93 Hapa siku moja wakati wasichana wengine walikuwa wakicheza na radiamu, nao wangeichovya, na kutia rangi mikono ya radiamu kwenye saa za mikono. Nina baadhi yake kwenye hii. Ndipo msichana mmoja akakosea na kuchukua brashi akaiweka kinywani mwake. Ikamwua. Basi miaka na miaka baadaye, walichukua darubini na kuiweka kwenye fuvu la kichwa la msichana huyo, na bado waliweza kusikia radiamu hiyo ikiendelea, "Burr-burr-burr." Haina kikomo. Inaendelea kufanya kazi, tena na tena. Haikomi.

94 Na, loo, ndugu, ikiwa radiamu ina athari ya namna hiyo ndani yetu, ni zaidi sana vipi Mwenyezi Mungu asiye na mwisho, wa Milele, wa kimbinguni, mwenye nguvu zote, asiye na kikomo! Yeye hana budi kuwa na matokeo yale yale aliyoanza nayo. Hana budi kuwa nayo kotekote, la sivyo, Yeye si Mwenyezi, Mungu mwenye nguvu zote. Angali anangojea mtu mwenye imani kakamavu, ambaye atatoka na kumpa adui changamoto juu ya msingi wa Neno Lake na kusema ya kwamba ndivyo lilivyo.

95 Na sasa ni nini kilichotokea, mara tu ule uamsho mkuu wa uponyaji ulipoanza? Ndipo maelfu ya askari, wa watu wa Mungu, waliobakia katika makanisa madogo, kama vile Oral Roberts, Tommy Hicks, na wengi wa hao watu wengine mashuhuri uwanjani, wakauchomoa Upanga wao wakaenda zao. Upanga *huu* unaokata kuja na kwenda pia, juu na chini, na

ndani na nje, “Mtambuzi wa mawazo, hata kwenye mafuta ya mfupa.” Walichomoa Biblia zao, Upanga wao, na kutoka nje, walipoona ya kwamba inawezekana. Nasi tumemshinda adui, kwa neema ya Mungu, mpaka ulimwengu mzima umekuwa na uamsho wa uponyaji. Inawezekana. Wachungaji wadogo waliokuwa na makanisa ya hali ya chini, na kadhalika, walishika moto na kuliona lile ono, wakauvuta Upanga wakaenda, na kumtukana adui.

96 Unajuaje wapo? Kuna watu mashuhuri, Mbunge Upshaw, Mfalme George wa Uingereza, na watu wengi wakuu waliokuwa hawawezi na walioteseka, wanaponywa kwa Nguvu za Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo hawawezi kusema lolote kuhusu hilo sasa. Imetendeka. Hakika! Alikuwa . . .

97 Kisha Eliya akaenda. Baada ya . . . Shauku ya moyo wake wote ilikuwa kupata ahadi hiyo. Alitaka ahadi. Hiyo ilikuwa ndiyo nia yake. Hiyo ilikuwa yote kwake. Hiyo ilikuwa ni maisha yake. Hiyo ndiyo ilikuwa kusudi lake, kila kitu. Yote, kila kitu, kilitegemea kuipata ahadi hiyo.

98 Nimeshawishika kuamini kwamba sisi sio waaminifu kwa jambo hili tunalozungumzia. Ikiwa nia yako yote, asubuhi ya leo, inategemea, “Kumpa Mungu sifa kwa ajili ya uponyaji wangu. Nimedhamiria kuponywa kwa Nguvu za Mungu. Nimeazimia kuishi maisha ya Kikristo. Nimeazimia kutembea kwa amani pamoja na Mungu. Nimedhamiria kufanya hivyo. Sijali yale mama anayosema, yale kanisa linayosema, yale mchungaji anayosema, yale mtu yeyote mwingine anayosema, yale ulimwengu unayosema. Nimedhamiria. Huo ndio umoja wa moyo wangu.” Utafika mahali fulani basi.

99 Ndipo, Elisha alipoona ya kuwa ameyakinia kuipata, Eliya alipoona kwamba *Elisha* aliyakinia, akampa ahadi. Sasa, ahadi ilikuwa, “Ikiwa unaweza kuniona ninapoenda! Ikiwa unaweza kuniona ninapoondoka!” Sasa imeachiwa Elisha. Alitaka kusikia ahadi, kwa hiyo akapata ahadi. Sasa kuna “ikiwa” ndani yake. “Ikiwa unaweza kuniona ninapoenda!”

100 Sasa, kama wewe ni mgonjwa asubuhi ya leo, nawe unataka kuponywa, ninaweza kukuthibitishia kwamba Kristo alikupa hiyo ahadi. Ahadi ni yako, “Ikiwa unaweza kuamini! Ikiwa unaweza kuamini!” Usishindwe.

101 Sasa Elisha alijivika vazi la Eliya, nabii. Ni mwendo wa mshindi ulioje! Jinsi alivyotembea, akikanyaga kwenda Mbinguni, kama mshindi! Alikuwa amesikia ahadi. Alihisi zile nguvu. Alikuwa akitembea kama shujaa, moja kwa moja kuelekea Yordani.

102 Mungu asifiwe, rafiki! Kila mwaminio, asubuhi ya leo, ambaye amejivika haki ya Kristo, anatembea kuelekea barabara ya Yordani. Hiyo ni sawa.

103 Acha mabomu ya atomiki yaje; yaachilie, kwa njia yoyote. Tumevikwa vazi na tunatembea, mshindi. Amina. Mimi. . . "Msiogope. Nimeushinda ulimwengu." Naam, bwana! Mkumbuke nini? "Nimeushinda ulimwengu." Kristo alisema hivyo.

104 Eliya alikuwa akitembea amevikwa vazi la kuachiwa, kama mshindi, kwa usahihi, akija Yordani.

105 Ndugu, hebu niseme hivi kwa heshima yako. Usivae vazi la mtu mwingine ambalo limeliwa kabisa na nondo wa mashaka, ambapo kushindwa huku kwote na ushirikina na hekaheka zimetoboa mashimo ndani yake, na linavuja kila mahali. Wewe vaa vazi la Mshindi, Kristo. Usilitumainie kanisa lako ambalo wakati mmoja lilifundisha wokovu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambalo wakati mmoja lilifundisha uponyaji wa Kiungu na sasa linaukana, lote limeliwa na nondo wa mashaka na kadhalika. Vaa vazi lake Yeye ambaye hajawahi kushindwa vita, kwa maana uko njiani ukielekea Yordani. Amina.

106 Sasa, alikuwa amevaa joho la kuachiwa, hiyo ni kweli. Na wengi wa watu asubuhi ya leo wamevaa majoho ya kuachiwa. Lakini alipofika Yordani, alitambua kwamba joho pekee lisingeweza kufanya kazi hiyo. Hiyo ni kweli. Nalo kanisa, Methodisti, Baptisti, Pentekoste, Presbiteri, "Loo, tuna shule! Kwa. . .Jamani, tunayo maadili yote, ya Biblia, chini sawia. Tuna joho lililofumwa vizuri kabisa, zile ahadi. Tunazo zote. Loo, tumebatizwa, tukazamishwa. Na sisi ni wa kimitume sana. Tumevaa imani ya kimitume. Tunaamini katika uponyaji wa Kiungu. Tunamwamini Mungu. Tunaamini katika Nguvu za Mungu. Tumebatizwa, katika Biblia, jinsi Biblia isemavyo. Tumempokea Roho Mtakatifu. Tumenena kwa lugha. Tunafanya yote hayo." Lakini, ndugu, kama hicho ndicho kitu pekee unachohitaji, utajikuta umepungukiwa, pia, utakapofika Yordani.

107 Loo, unaweza kuwa umefundishwa. Unaweza kuwa mwerevu. Unaweza kuwa na D.D., Daktari wa Kiungu. Unaweza ukawa na Ph.D., Daktari wa Falsafa. Unaweza kuwa na LL.D., Daktari wa Kilatini. Unaweza kuwa na digrii za kila namna. Unaweza kuwa umevikwa joho la kanisa la Methodisti. Unaweza kuwa umevikwa joho la kanisa la Kipentekoste. Unaweza kuwa umevikwa joho la Assemblies, au Umoja, au Wautatu, ama lolote lile. Ni joho la kuachiwa tu, kwanza kabisa, hiyo ni kweli, la mafundisho fulani ya sharti ya kujibunia, yaliyowaziwa, na kadhalika namna hiyo; na hata kama umekuwa Mkristo, na hilo kanisa limekuwa la Kikristo, na limevalia kwa usahihi.

108 Lakini wakati Elisha, aliposimama, akionekana wazi, kwenye ufuko uliojaa manabii na wakosoaji, wakiona atakalofanya, naye huyu hapa anakuja, akitembea amevikwa joho la Eliya, loo, jamani, haleluya, amesomeshwa vinginevyo,

amesoma, amejitolea, anaamini, hana kasoro yoyote, anashuka kuja Yordani, ulimwengu unamwangalia.

109 Ee Mungu, jinsi tunavyohitaji hilo siku hizi! Kukiweko na wasomi wengi waliosoma na wenye elimu; pamoja na watu wengi wanaoweza kuichambua Biblia hiyo na kuiweka pamoja, katika hisabati; watu wengi wanaoweza kufanya mambo makuu katika fani za kufundisha; wanaoijua historia ya Biblia kikamilifu, wanaoweza kukwambia saa ambayo mshumaa uliwashwa, na saa ulipozimika. Wanaweza kukwambia mambo haya yote. Nao wana . . . Wana ubatizo wa maji. Wana ubatizo wa kiroho, kama wanavyouita, joho. Wameweka kila kitu katika utaratibu.

110 Vivyo hivyo na Eliya. Lakini alipofika Yordani, kuukabili ulimwengu mkosoaji, alilia nini? “Yuko wapi Mungu wa Eliya?” Halikuwa ni joho la Eliya lililofanya jambo hilo. Ilikuwa ni Nguvu za Mungu wa Eliya, ndizo zilizofanya hilo.

111 Basi kitu ambacho ulimwengu unahitaji asubuhi ya leo ni Nguvu za Mungu wa Eliya. Huenda umenena kwa lugha na kupaza sauti, na kukimbia sakafuni. Lakini tunachohitaji ni Nguvu za Mungu wa Pentekoste, kutoa maisha na mambo yaliyoishiwa siku hizo, katika nguvu za kimitume.

112 Joho la kuachiwa lilikuwa sawa, lakini alihitaji wito mpya moyoni mwake kutoka kwa Mungu. Alihitaji upako mpya kutoka kwa Mungu. Alikuwa amevaa joho la kuachiwa alipofika mtoni, bali alihitaji wito mpya kabisa wa kwanza kutoka kwa Mungu, na Nguvu za kwanza kutoka kwa Mungu, kufanya huo muujiza.

113 Basi, ndugu yangu, usiogope kumwomba Mungu chochote. Ni lazima umdai Mungu, au umwombe Mungu, chochote ambacho ameahidi. Kwa maana, ikiwa ninamtambulisha Mungu ambaye yuna nguvu zote na mweza yote, na ikiwa mimi ni mtumishi wa Mungu, sina budi kufanya kazi za Mungu. Na kama nikizifanya kazi za Mungu, sina budi kumwomba Mungu ayatimize mambo haya, kwa sababu ananitaka nifanye yasiyowezekana. Sina budi kumwomba. Sina budi kumwita, na kusimama hapo na kusema, “Mungu, uliahidi jambo hilo.” Vivyo hivyo na wewe, kila mtu.

114 “Mtapokea nguvu,” Matendo 1:8, “akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu.” Roho Mtakatifu akiisha kuwajilia juu yenu! Ukiisha kuvikwa kama Mkristo, imani yako ikiisha kuwekwa ndani ya Kristo, ndipo utapokea nguvu. Haya basi. Naam.

115 Na, ndugu, dada, kila mmoja wenu, asubuhi ya leo, naomba niseme jambo hili kabla ya kuwaombea wagonjwa, naomba niseme hivi: Kwa msaada wa Mungu, niombeeni. Niliposimama, miaka kumi iliyopita, kwenye jukwaa hili, nikihubiri juu ya Daudi na Goliathi, sasa si Goliathi aliyenizuia, Mungu amemwangamiza mbele zangu, lakini jambo ambalo limenizuia,

ni ukosefu wa imani, ukosefu wa kitu ambacho nilijua kilikuwa huku karibu.

116 Na asubuhi ya leo, mbele ya maskani hii ndogo tena, ninapaza sauti: yuko wapi Mungu aliyetoa ahadi hii? Yuko wapi Mungu aliyenikuta na hii, huko ng'ambo? Jitokeze, Mungu, na unipe ujasiri. Nipe nguvu. Nipe nia thabiti, bila kujali kijacho au kiendacho. Kama kunaonekana giza, au kama kunaonekana . . . Hata kuonekaneje, songa mbele. Ahadi ni ya kweli.

117 Na ndugu, dada, moja ya siku hizi . . . Kwenu ninyi marafiki wenye dhambi hapa asubuhi ya leo, na kwenu ninyi watu mnaojaribu kuiga Ukristo, unaweza kuwa mfuasi wa kanisa, hiyo ni sawa kabisa, sina la kusema dhidi ya hilo, sina neno dhidi ya elimu yako nzuri ya kitaalamu, au dhidi ya theolojia yako, sina neno dhidi ya hilo, lakini, loo, yuko wapi Mungu?

118 Haikuwa ni Eliya, hata hivyo. Eliya siye aliyeufungua mto huo. Haikuwa ni joho lake. Elisha alilitoa begani mwake. Alilikunja vile vile tu Eliya alivyolikunja. Lakini alipoanza kujaribu kulipeperusha, hapakuwa na Nguvu pale. Ndipo basi akalia, akijua kwamba Mungu alikuwa mahali fulani, "Yuko wapi Mungu huyo? Yuko wapi?" Basi hapana shaka kitu fulani kilimgusa huyo nabii, kwa maana alilipeperusha vazi hilo na kuyapiga maji, nayo yakafunguka huku hadi huku. Na mbele ya makasisi wa siku hizo, mbele ya wakosoaji wa siku hizo, akavuka Yordani, kama tu Eliya alivyotangulia kufanya.

119 Hatuhitaji mafundisho; tunayo hayo. Lakini tunamhitaji Mungu wa Eliya. Tunahitaji Nguvu za Mungu wa Eliya, zirudi kanisani mwetu. Nguvu za kulifanya lishikilie hapo, na kuliita Neno la Mungu, "Kweli," haidhuru.

120 Nasi, kila mtu hapa asubuhi ya leo, kama wanadamu, tuko njiani kuelekea Yordani. "Naye alipofika Yordani." Utafika huko, moja ya asubuhi hizi au moja ya siku hizi usiku.

121 Alipofika Yordani, alikuwa akitembea kama mshindi. Lakini, alipofika Yordani, hiyo ilikuwa ndiyo tofauti. Alikuwa amevaa joho la kuachiwa. Mtu mwingine alikuwa amelivaa. Lakini lilikuwa ni joho zuri, naye alijua yule mtu aliyevaa joho hilo alikuwa ni nani.

122 Ndugu, dada, moja ya asubuhi hizi, sina budi kushuka Yordani.

123 Nilikuwa nikiwazia. Alasiri ya leo, tunaenda huko kwa Ndugu na Dada Wright. Msiwasahau. Haya ni maadhimisho ya miaka hamsini ya arusi yao. Ninaamini, kanisa, litakula cha—chakula cha jioni pamoja nao. Nilikuwa nikiwazia, hivi majuzi: miaka hamsini! Nami ninawaangalia wote wawili, wazee sana na wamedhoofika. Nikawazia, "Ndiyo, nina umri wa miaka arobaini na saba." Walioana miaka mitatu tu kabla ya mimi kuzaliwa.

124 Arobaini na saba! Ninatembea kuelekea Yordani. Sina budi kushuka. Sina budi kufika huko. Nitafika huko. Huenda ikawa ni katika ajali ya barabarani. Huenda nikaanguka kutoka angani, kwenye ndege. Huenda nikachomwa, kwa mshale wa ibilisi mahali fulani, nikafa. Sijui ninavyoenda. Lakini, kuna jambo moja ninalojua, ninaenda, na ninatembea kuelekea Yordani.

125 Lakini nitakapofika huko, ninataka kujua jambo moja, ya kwamba nimevikwa joho la kuachiwa, pia. Sitegemei langu, kwa sababu si zuri. Kwa maana, mara tu Eliya alipoliokota joho la Elisha, alilirarua vazi lake vipande-vipande na kulitupa chini. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa nilipompata Kristo. Nilijirarua mwenyewe, mawazo yangu mwenyewe, upuuzi wangu mwenyewe, kitu changu kidogo. Niliwazia, nilipokuwa mdogo, mhubiri wa Kibaptisti, nilikuwa kama tu . . . Nilikuwa mtu mashuhuri. Lakini, niliirarua; nikavaa vazi Lake. Ndipo nitakapofika Yordani, nataka kujiona nimevikwa vazi Lake. Atafuata hilo. Nasi tutafika huko siku moja.

Lakini hebu na tuombe kwa muda kidogo tu.

126 Baba wa Mbinguni, tukiwa kwenye safari yetu ya kwenda Yordani asubuhi ya leo, kama washindi, na siku moja, hatuna budi kuwasilisha kitu fulani Yordani, hiyo ni, kufa. Na, loo, litakuwa ni jambo la kutisha jinsi gani, kutengwa na Mungu. Hatuwezi kuvuka. Hapana. Lakini, Eliya, alipofika huko, alikuwa amevaa vazi la Elisha . . . vazi la Eliya. Ndipo alipolivua hilo vazi . . . la Eliya, mtu ambaye alikuwa amependeza machoni Pako, nawe ulikuwa umemkubali na ukampandisha Mbinguni pamoja Nawe. Naye Elisha alikuwa amevaa vazi lake, kwa hiyo akawasilisha Yordani, kifo, vazi la Eliya. Nalo likakubalika, ndipo Yordani ikafunguka, naye akavuka.

127 Mungu mpendwa, siku moja, hatuna budi kushuka. Hatuwezi kuwasilisha matendo yetu mema; hatuna yoyote. Hatuwezi kuwasilisha chochote duniani. Hata sitamani kitu chochote, kujaribu kuwasilisha, lakini ninatumainia kabisa ustahilifu wa Yesu. Ulimkubali, na ukamfufua kutoka kwa wafu, Naye akaletwa Uweponi mwa Mungu na hapo atadumu milele. Basi, Mungu, ninataka kuwasilisha hilo Kwako, ya kwamba ninamwamini Yeye, na ninampenda. Na, kwa neema Yake, ametuvika joho Lake. Nami naomba, Baba, ya kwamba utatusaidia sasa katika siku za vita. Na ambapo watu wa Mungu wanapaswa kufanya kazi za Mungu, naomba ya kwamba utaturuhusu tuchukue joho la Kristo, nguvu za Roho Mtakatifu, na kumwita Mungu aliyeishi ndani Yake. Lijalie. Katika Jina la Kristo tunaomba.

128 Na huku tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu. Ninashangaa tu, hapa asubuhi ya leo, kama kuna mtu ambaye anajaribu kushuka kwenda Yordani, bila joho hili. Ikiwa kuna mtu ambaye

hajavikwa joho la Yesu Kristo, na ingawa lilivaliwa wakati mmoja na Mwana wa Mungu. Sijui, kama huna hilo asubuhi ya leo, kama ungeinua mikono yako kwa Mungu na kusema, "Mungu mpendwa, saa hii, sasa nataka kulikubali."

129 Mungu akubariki, mama. Je, mtu mwingine, waweza kuinua mkono wako? Mungu akubariki, mwanangu. Mtu mwingine, waweza kuinua tu mkono wako? Mungu akubariki, mvulana mdogo. Mungu akubariki, kijana. Mtu mwingine angeinua mkono wao? Mungu akubariki, huko nyuma, bwana.

130 Sema tu, "Kwa msaada wa Mungu, asubuhi ya leo, nataka kuachana na kujiona kuwa mwenye haki, mawazo yangu mwenyewe, na fikira zangu za anasa na burudani, na dhambi ambayo nimeishia. Nami nataka Kristo anivike joho Lake, asubuhi ya leo, nipate kulitumia joho Lake. Najua ni kamilifu." Mungu akubariki, mwanangu. Mtu mwingine aseme, "Na nitainua tu . . . "

131 Inua mkono wako, useme, "Sasa nataka kumkubali Roho Mtakatifu maishani mwangu. Ninataka kuvikwa haki Yake. Nitakapofika huko siku hiyo, sitajiwasilisha na kusema, 'Vema, sasa, najua nilimnunulia mtu fulani makaa. Nilifanya hivi.'" Hiyo ni nzuri, ni nzuri sana, lakini hiyo . . . Ilibidi kitu fulani kife, upate kuishi, na ni kupitia kwa tendo hilo tu unaweza kuokolewa. Je, utainua mkono wako? Useme, "Kristo, sasa naiacha njia yangu mwenyewe. Ninaikubali njia Yako. Nataka unirehemu nitakapofika mwisho wa safari?" Vema. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Vema.

Sasa tunaenda kuomba.

132 Sasa, Baba wa Mbinguni, Mwenye Haki, kama mikono saba, minane, kumi imeinuliwa. Sijui hali yao. Wewe wajua yote kuwahusu. Sijui mimi. Lakini wana haja leo. Na wanatambua kwamba ni wahitaji, na wako tayari kuja na kukubali msaada wakati wa shida; kuona kwamba, ile saa kuu inayokaribia sasa, yale mabomu ya atomiki, mambo makuu ambayo yanatungojea.

133 Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Wewe utawabariki watu hawa, na leo hii uweke mkono Wako juu yao na uwaondolee maovu na mashaka yao yote. Na ujalie walitupilie mbali vazi lao kuukuu lililoliwa na nondo wa kujihesabia haki, ambapo parare na nyenje, na nondo wa ushirikina na ukanisa, wamekula wakatoboa mashimo ndani yake, na (wao) halitashikilia tena. Jalia tu walitupilie mbali, na kunyoosha mkono na kulitwaa vazi la Bwana Yesu. Waseme, "Ninamtumaini Yeye. Ninajivika mwenyewe, si kwa haki yangu, wala kwa mawazo yangu mwenyewe. Lakini, tangu saa hii na kuendelea, ninakutumaini Wewe." Jalia kwamba watalipokea, Baba, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

*Joho La Kuachiwa* SWA56-1125M
(A Secondhanded Robe)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 25 Novemba, 1956, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani  kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org